**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 8 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA**

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ya Spika imetolewa chini ya Kanuni ya 39(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria saba ifuatayo:-

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024);*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2024 *(The written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2024);*

Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024;

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi za Mwaka 2024 *(The Labour Laws Amendment Bill, 2024)*;

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 *(The Environmental Management Amendment Bill, 2024);*

Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi wa Mwaka 2024; na

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Fedha za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 *(The Supplementary Appropriation for the Financial year 2024/2025.*

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii ninapenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo saba imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwa Sheria za nchi zinazoitwa: *(Makofi)*

Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.1) ya Mwaka 2025 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No.1, 2025)*;

Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) ya Mwaka 2025 *(The written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 2, 2025)*;

Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania (Na.3) ya Mwaka 2025;

Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi (Na.4) ya Mwaka 2025 *(The Labour Laws Amendment Act No. 4, 2025);*

Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (Na.5) ya Mwaka 2025 *(The Environmental Management Amendment, Act No. 5, 2025)*;

Sheria ya Uwekezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (Na. 6) ya Mwaka 2025; na

Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Nyongeza ya Fedha za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Na. 7) ya Mwaka 2025 *(The Supplementary Appropriation for the Financial Year 2024/2025) (Act No. 7, 2025.))*

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, Spika. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kama ifuatavyo:-

(i) Fungu Na. 25, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;

(ii) Fungu Na. 37, Ofisi ya Waziri Mkuu;

(iii) Fungu Na. 27, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;

(iv) Fungu Na. 61, Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(v) Fungu Na. 92, Tume ya Kudhibiti Ukimwi;

(vi) Fungu Na. 92, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;

(vii) Fungu Na. 42, Mfuko wa Bunge;

(viii) Fungu Na. 15, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi; na

(ix) Fungu Na. 65, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Viti Maalum.

Na. 1

**Ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Isansa – Magamba hadi Mkwajuni Wilaya ya Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mlowo – Isansa – Magamba hadi Mkwajuni Wilaya ya Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa ajili ya kuiboresha Barabara ya Mlowo – Isansa – Magamba hadi Mkwajuni ambapo katika mwaka 2019/2020, Serikali ilipeleka shilingi 294,630,000.00 kwa ajili ya kufungua barabara hii kipande chenye urefu wa kilomita 16.2 eneo la Magamba hadi Ilumbwe. Aidha, katika mwaka 2022/2023, Serikali ilitumia shilingi 75,684,400.00 kujenga *Solid Drift* safu mbili, *box* kalavati kubwa moja *(two cells)* na mifereji ya maji ya mvua mita 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024, Serikali imetumia shilingi 365,395,000.00 kufanya matengenezo ya barabara kipande chenye urefu wa

kilomita 13.1 kuanzia Mlowo hadi Isansa ambazo zimefanya kazi ya kuumba tuta la barabara kilometa 13.1, kuweka changarawe na kushindilia, kujenga safu saba za kalavati pamoja na kujenga mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 1085.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuiboresha barabara hii kwa kuijenga na kuifanyia matengenezo mara kwa mara ili kuiimarisha zaidi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii wananchi wa Wilaya ya Songwe wamekuwa wakikutana na changamoto nyingi sana hasa wanapokuwa wanahitaji huduma makao makuu ya mkoa. Inawalazimu kupitia Mkoa mwingine wa Mbeya kabla ya kufika Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe. Sasa, ninataka kujua ni lini Serikali itakamilisha barabara hii ili kuepusha adha ya gharama na muda kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu namba mbili, ninataka kujua ni lini watafanya marekebisho makubwa kwa kipande cha Barabara kutoka Isongole – Itumba Wilayani Ileje hasa ukizingatia kwamba barabara hii imebeba sura halisi ya makao makuu ya wilaya? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali zuri kabisa la Mheshimiwa Mbunge. Kwanza ninampongeza kwa nia yake thabiti ya kutaka kuwapambania wananchi ili waweze kupata barabara nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na Barabara hii ya Mlowo – Isansa – Magamba kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilitenga bajeti ya shilingi 344,650,000 kwa ajili ya kukarabati kipande cha kilomita 13.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na umuhimu mkubwa wa barabara hii tayari mkoa kupitia kikao chake cha Bodi ya Barabara kilichoketi Machi 2024, umeomba idhini kwa ajili ya Barabara hii ya Mlowo – Isansa – Magamba kupandishwa hadhi kuwa miongoni mwa barabara zitakazohudumiwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, Barabara hii ya Isongole – Itumba ni barabara ambayo inahudumiwa na *TANROADS*. Kwa hiyo, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi ili kuhakikisha miundombinu hii inaweza kupatiwa fedha na kutengenezwa katika viwango ambavyo vitawanufaisha wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mji wa Babati zimeharibika sana, tangu mwaka jana *TARURA* hawajapewa fedha. Ni lini *TARURA* watapewa fedha ili watengeneze barabara hizo? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Gekul kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya jitihada thabiti kabisa kwanza kuongeza bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 275 mpaka sasa kila mwaka *TARURA* ina bajeti ya shilingi bilioni 710.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha barabara hizi za wilaya zenye umuhimu mkubwa sana kwa wananchi kiuchumi na kijamii zinaweza kujengwa na fedha zinatoka kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge fedha zinaendelea kutoka na zitafika kwenye jimbo lake

kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi zenye umuhimu mkubwa sana kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itakarabati Barabara ya Mahenge – Mwaya – Ketaketa ambayo ni mbovu sana? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za wilaya ambazo zinawasaidia wananchi kiuchumi na kufikia huduma za kijamii. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kuhakikisha inazifikia hizi barabara, inaongeza mtandao mrefu zaidi wa barabara zenye hadhi ya juu zaidi ikiwemo hadhi ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hata katika eneo hili alilolitaja Serikali itaendelea kuleta fedha kuhakikisha inakarabati na kujenga barabara hizi ili ziweze kuwanufaisha wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kuishukuru Serikali kwa kutujengea kilomita moja ya lami pale Makao Makuu Karumwa. Hata hivyo, barabara ile imejengwa na kunyanyuliwa juu na zile nyumba zilizoko pembezoni kuonekana kuwa chini. Mvua inaponyesha maji huingia kwenye nyumba za watu. Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga mifereji na kuzuia adha hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Hussein Amar kwa kutaka kuona wananchi wake wanapata miundombinu mizuri

ikiwemo mifereji kwa ajili ya kupokea maji ya mvua na kutokuleta adha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya jitihada hizo na ndiyo maana kila mwaka inatenga fedha kwa ajili ya kukarabati barabara zetu hizi ambazo zinahudumiwa na *TARURA*. Serikali itafika katika eneo hili ili kuweza kujenga mifereji hiyo ili iweze kuwanufaisha wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ninavyoongea hapa Barabara za Tarafa ya Mamba - Vunta na Gonja ambazo ni barabara za milimani zinazowafanya wananchi wateremke tambarare zote zimekufa. Je, lini Serikali itaziangalia hizi barabara kwa haraka ili wananchi wa milimani waweze kufikisha mazao yao kwenye masoko madogo na makubwa ambayo yako tambarare? Ninaomba jibu la uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Anne Kilango kwa swali hili ambalo linalenga kuwaletea wananchi wake maendeleo…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaomba utulivu Bungeni. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Anne Kilango kwa swali lake zuri ambalo linalenga kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie kwamba jitihada za Serikali zinafanyika kuhakikisha inafikia mtandao mkubwa zaidi wa barabara hizi zinazohudumiwa na *TARURA* ili kuweza kuwanufaisha wananchi. Kwa hiyo, ninaomba

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafika katika tarafa hizi alizozitaja kwa ajili ya kuhakikisha inarekebisha barabara hizi, inazijenga katika kiwango ambacho hakitawakwamisha wananchi wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Balozi Liberata.

Na. 2

**Zahanati ya Kakoni - Misenyi kutoa Huduma**

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Zahanati Kitongoji cha Kakoni - Misenyi ili iweze kuhudumia wananchi wa Kitongoji hicho na jirani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na ujenzi wa zahanati katika vijiji na mitaa inayokidhi vigezo ili kusogeza huduma za afya ya msingi karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025, Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi imepelekewa jumla ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwongozo wa Serikali wa Ujenzi wa Vituo vya kutolea Huduma za Afya ngazi ya msingi unaelekeza ujenzi wa zahanati kwenye ngazi ya kijiji. Aidha, Kakoni ni miongoni mwa Kitongoji katika Kijiji cha Kitobo ambacho tayari kina zahanati. Hivyo, kwa mujibu wa mwongozo, Kitongoji cha Kakoni kitahudumiwa na Zahanati ya Kitobo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Liberata.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, kitu ambacho nilitaka kujua ni kwamba, ni lini kituo kidogo cha afya kilichopo katika hicho Kitongoji kitaweza kuongezewa hadhi kuwa zahanati kwa maana ni kituo ambacho kitahudumia karibu vitongoji nane vya Kakoni, Musibuka, Luweru, Lushasha, Nyabutaizi na vingine vingi kwa sababu kile ulichokitaja kiko mbali sana? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Huduma za Afya Msingi, ujenzi wa zahanati unafanyika kwenye kijiji kinachokidhi vigezo, lakini pia kwenye mitaa ambayo inakidhi vigezo. Kwa hiyo, kwa sababu tayari katika Kijiji hiki cha Kitobo tayari kuna zahanati, naomba tu nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaendelea kufanya tathmini kuona umbali wa Kitongoji hicho cha Kakoni ambacho kiko ndani ya Kijiji cha Kitobo na ikiwa kutakuwa na ulazima wa kujenga zahanati, basi tutawasiliana na halmashauri ili taratibu zianze. Hata hivyo, kwa sasa kwa mujibu wa Sera, kitongojii hicho kitapata huduma ndani ya Kijiji cha Kitobo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itajenga Wodi ya Mama na Mtoto katika Zahanati ya Funvuhu iliyopo kwenye Kata ya *Old* Moshi Mashariki, kwa sababu iliyopo kwa sasa haikidhi vigezo? Ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya tathmini na kuainisha zahanati zote na hususani zahanati zile zilizojengwa miaka 20 iliyopita, ambazo majengo yake yalikuwa madogo na yalikuwa hayana chumba kikubwa kinachotosheleza huduma za uzazi (Wodi ya Wazazi).

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hiyo zahanati tutaiingiza kwenye mpango wa kupanua ili kupata jengo kwa ajili ya mama wajawazito kupata chumba cha kujifungulia na kuboresha zaidi huduma za afya katika eneo hilo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Runyala, Kanazi na Kakoma viko mbali na Hospitali ya Wilaya, hawana Vituo vya Afya na wamekwishaanza jitihada za kujenga zahanati. Ni mkakati upi wa Serikali wa kupeleka fedha ili kuweza kujenga zahanati hizo? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, kufanya tathmini katika vijiji hivyo vya Kanazi na hivyo vijiji vingine ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Pia, ikiwa vinakidhi vigezo vya kujengewa zahanati, halmashauri ianze kukusanya mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kushirikiana na nguvu za wananchi. Vilevile na sisi Serikali Kuu tutaanza kuweka kwenye mpango wa bajeti kwa awamu ili kujenga zahanati hizo na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi hao. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeleta vifaatiba kama vile *X- ray* na *Ultrasound* kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika na vituo vyote vya afya na hatuna mtaalam kwenye eneo hilo; je, ni lini Serikali italeta mtaalam wa mionzi ili aweze kufanya kazi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika pamoja na vituo vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Ni kweli kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele cha hali ya juu sana katika upatikanaji wa vifaatiba vya kisasa katika zahanati na hospitali zetu zote za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Tanganyika imepata vifaatiba vya kutosha ikiwemo *digital x-ray*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kushirikiana na wadau, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya, tumeanzisha programu maalum ya mafunzo ya muda mfupi ya wataalam wa *X- Ray* na *Ultrasound* na mara watakapokuwa wamehitimu tutawapeleka kwenye vituo vyetu vyote vyenye upungufu ikiwemo Kituo cha Afya katika Halmashauri hiyo ya Tanganyika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, kwenye swali la kwanza, la pili na la tatu, nina maswali ya nyongeza 18 ya Wabunge kwa maandishi. Niwahakikishie kuwa hoja zenu zote zitatimizwa na Serikali mpaka mwezi Juni. Ahsante sana na tunaendelea. Mheshimiwa Ally Juma Makoa.

Na. 3

**Fedha za Ujenzi wa Miundombinu ya Vituo vya Afya Kolo, Mongoroma na Kingale**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, lini fedha za ujenzi wa majengo ya *x-ray, OPD*, wodi za wagonjwa, *mortuary*, kuchomea taka, kufulia na *walk ways* zitapelekwa Vituo vya Afya vya Kondoa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya nchini, ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 shilingi bilioni 107 zimetolewa na kujenga vituo vya afya 367 kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa upungufu wa miundombinu katika Vituo vya Afya vya Serya, Kolo na Kingale vilivyopo katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa. Kituo cha Afya Serya kina upungufu wa miundombinu ya wodi za kulaza wagonjwa, jengo la mionzi pamoja na jengo la kuhifadhia maiti. Kituo cha Afya Kolo hakina jengo la kufulia, jengo la mionzi, njia za kutembelea wagonjwa na kichomea taka. Pia, Kituo cha Afya Kingale hakina jengo la mionzi, njia za kutembelea wagonjwa pamoja na wodi za kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa miundombinu ya majengo haya katika vituo vyetu vya afya, itaendelea kufanyika kwa awamu kote nchini vikiwemo Vituo vya Afya Kolo, Kingale na Mongoroma katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; sasa, kwa kuwa miundombinu hii ni muhimu sana na wagonjwa wanapokosa miundombinu hii wanalazimika kuletwa Hospitali ya Wilaya kwa tabu sana. Pia, kwa sababu vituo vyote hivi vya afya havina *ambulance*, Serikali inasemaje kuhusu kutupatia *ambulance* kwa ajili ya kuhudumia vituo hivi wakati tukisubiria fedha za kukamilisha miundombinu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; niliomba Kituo cha afya kile cha Jimbo cha Kimkakati kujengwa Kondoa Mjini. Je, ni lini Serikali Serikali itatuletea fedha hizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, vituo hivi vya afya ambavyo ameviwasilisha yeye mwenyewe Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambavyo vina upungufu wa miundombinu hii tayari tumeanza kuviweka kwenye mpango kwa ajili ya kukamilisha miundombinu hiyo kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumwelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa, kuna baadhi ya miundombinu kwa mfano *walkways* ziko ndani ya uwezo wa mapato ya ndani ya halmashauri. Kwa hiyo, wahakikishe kwenye bajeti zao za ndani wanatenga fedha kwa ajili ya kujenga *walkways* za kutembelea wagonjwa wakati Serikali Kuu ikiandaa fedha kwa ajili ya kwenda kujenga miundombinu hii ambayo inahitaji gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na magari ya wagonjwa. Ni kweli Halmashauri ya Mji wa Kondoa imepata pia magari ya wagonjwa, lakini tunafahamu kwamba bado ina uhitaji mkubwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kupeleka magari hayo kwa ajili ya vituo hivyo ambavyo havina magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kimkakati. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshaainisha kata zote za kimkakati ambazo Waheshimiwa Wabunge waliwasilisha na tayari tuko kwenye hatua ya Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuwasilisha fedha hizo kwenye kata hizo kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Lushoto, Kituo cha Afya Lunguza kimejengwa kwa awamu ya kwanza na bado awamu ya pili ambayo yanahitajika

majengo ya *mortuary*, chumba cha upasuaji na jengo la *X- Ray*. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha kituo hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali ilishapeleka fedha katika Halmashauri ya Lushoto, Jimbo la Mlalo, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata hiyo ya Lungunza ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimhakikishie kuwa Serikali inatambua kwamba majengo yaliyojengwa ni ya awamu ya kwanza na tunahitaji fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu umuhimu wa jengo la upasuaji, wodi pamoja na majengo mengine na tayari tutaweka kwenye mpango wa bajeti kwa ajili ya kwenda kumalizia majengo hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Ezra.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa watu wa Sirari na Nyamwaga kupata *X-Ray machine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Nyamongo kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 ina zaidi ya watu 60,000. Vilevile, Vituo vya Afya Sungusungu, Nyamongo na Kerende hawana *X-Ray Machine*. Ni lini Serikali itapeleka *X-Ray machine* ili kusaidia watu wa Nyamongo wasiumie sana hasa kwenye machimbo ya mgodi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika vigezo vya kipaumbele katika kupeleka vifaatiba ni pamoja na idadi ya wananchi. Pia, kwa kuwa Kata hiyo ya Nyamongo ina wananchi takribani 60,000 ina kila sababu ya kupata mashine ya *X-Ray*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaiweka kwenye mpango kwa ajili ya kupeleka *X-Ray* katika Kituo hicho cha afya. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo umekamilika na unaendelea vizuri na wananchi wanapata huduma. Hata hivyo, yako maombi yetu ya jengo la *theatre*, wodi ya wanaume, *walkways* pamoja na kichomea taka. Je, ni lini ile pesa shilingi milioni 750 itafikishwa pale ili kila kitu kiweze kukamilika na wananchi wapate huduma kikiwa kimekamilika? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Chiwelesa kwamba ujenzi wa Hospitali zetu za Halmashauri na vituo vya afya huenda kwa awamu na tumejenga majengo kadhaa katika Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo na ninafahamu kwamba kuna upungufu wa majengo hayo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Biharamulo, kwamba Serikali inatambua na itakwenda kukamilisha majengo yaliyobaki ili tuweze kutoa huduma zote muhimu kwa ngazi ya hospitali katika Halmashauri ya Biharamulo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Vita Kawawa.

Na. 4

**Hitaji la Magari ya Kubebea Wagonjwa Vituo vya Afya Lusewa na Magazini**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itavipatia Magari ya kubebea wagonjwa Vituo vya Afya vya Magazini na Lusewa – Namtumbo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilinunua magari 594 ya kubebea wagonjwa na usimamizi wa huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari haya yamesambazwa kwenye Halmashauri kwa wastani wa magari mawili hadi manne kwa kila Halmashauri, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imepokea magari mawili ya kubebea wagonjwa. Magari hayo yanatumika katika Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo na Kituo cha Afya cha Mtakanini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mipango ya kununua magari ya kubebea wagonjwa kwa ajili ya vituo vya afya nchini vikiwemo Vituo vya Afya vya Magazini na Lusewa – Namtumbo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Vituo hivi vya Afya viwili, kimoja cha Magazini kiko kilometa 254 mpaka kufikia Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya na hiki cha Lusewa kiko kilometa 220 mpaka kufikia Makao Makuu ya Wilaya. Vilevile, kuna kingine cha Ligela kiko kilometa 110. Je,

Serikali iko tayari kutuletea hayo magari ya vituo vya afya vilivyo mbali kabisa na makao makuu ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Kata za Kimkakati za Namabengo, Mgombasi na Mchomolo nazo zina uhitaji wa vituo vya afya. Pia, Mheshimiwa Rais alipopita Namtumbo tarehe 27 mwezi Septemba, wananchi wa Mchomolo walimwomba kituo cha afya eneo hilo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, twende kwenye swali.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Waziri wa TAMISEMI, alikubali. Je, ni lini watawaletea fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mchomolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo Serikali imepeleka magari ya wagonjwa mawili katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, tunatambua pia uhitaji wa magari hayo katika Kituo cha Afya cha Magazini na Lusewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, safari ni hatua na tunakwenda kwa awamu. Tumepeleka magari mawili mapya ndani ya miaka miwili. Vilevile, tutahakikisha pia tunapotenga bajeti nyingine kwa ajili ya magari ya wagonjwa, tutatoa kipaumbele kwenye vituo hivi vya afya ambavyo viko mbali sana kutoka Hospitali ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele namba moja kwenye utekelezaji wa bajeti zetu. Pia, tunafahamu kwamba ni maelekezo yake kuwa tupeleke Kituo cha Afya Kata ya Mchomolo. Pia, nimhakikishie Mbunge tayari tumeingiza kwenye Mpango wa Bajeti mwaka 2025/2026 kupitia *World Bank* ili kuhakikisha Kituo hicho cha Afya kinajengwa pale Mchomolo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Afya vya Mziha, Mvomero, Melela na Mlali, hawana magari ya kubebea wagonjwa. Je, lini Serikali itapeleka magari ya kubeba wagonjwa katika vituo hivi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, Serikali inapeleka magari ya wagonjwa katika vituo vya afya na hospitali za halmashauri. Hata hivyo, kwenye vituo vya afya si kila kituo cha afya lazima kiwe na gari la wagonjwa. Kwa sababu, Kituo cha afya kimoja kinaweza kikawa na *satellite facilities* tatu au nne kwa ajili ya kutumia lile gari moja la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Jonas, kwamba tumepokea mahitaji hayo ya vituo hivyo vya afya kupata magari ya wagonjwa na tutakwenda kuyafanyia kazi ili kuona angalau kimoja au viwili ambavyo vinaweza vikahitaji gari la wagonjwa mbali na vituo vyote ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

Na. 5

**Kukamilisha Ujenzi wa Zahanati ya Mangio**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa zahanati iliyoboreshwa ya Mangio iliyopo Kata ya Mwaniko, Wilayani Mwanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Mangio ilianzishwa kwa nguvu za wananchi mwaka 2010 na baadaye kuendelea kukamilishwa kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri, Serikali Kuu na Mfuko wa Jimbo ambapo jumla ya shilingi milioni 74 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hiyo, ambapo kwa sasa iko 85% ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imetenga shilingi milioni 20 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Mangio. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na ahadi hiyo ya kutenga fedha za halmashauri, ninaomba tu niulize swali moja. Kwa kuwa Halmashauri ya Mwanga ni moja kati ya halmashauri zenye changamoto kubwa sana ya mapato. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa upendeleo kwa zahanati hii ambayo imekuwa bila kukamilika kwa muda mrefu sana kiasi ambacho imeanza kuharibika sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu na Mheshimiwa Mbunge ametolea hoja kuhusu Zahanati ya Mangio mara kadhaa na imechukua muda mrefu kukamilika tangu mwaka 2010 hadi sasa. Hata hivyo, nimhakikishie tu kwamba, kwa sababu tayari Serikali Kuu ilishapeleka fedha, lakini na yeye mwenyewe kupitia Mfuko wa Jimbo jumla ya milioni 74 na tayari halmashauri kwa mwaka ujao wa fedha 2025/2026 imetenga milioni 20. Tuna uhakika kwamba, katika mwaka huu wa fedha mapema, zahanati hii itakamilishwa na wananchi wataanza kupata huduma zilizokamilika katika ngazi ya zahanati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Pale kwenye Kijiji cha Ngwale kwenye Kata ya Gwata, wananchi wameanza ujenzi wa zahanati kwa nguvu zao. Je, ni lini Serikali itawaongezea nguvu ili waweze kukamilisha zahanati hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza wananchi wa Gwata kwa kuanza ujenzi wa zahanati kwa nguvu zao. Pia kwa kadri ya mwongozo wakifika hatua ya lenta, tutahitaji taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili iweze kuingizwa kwenye bajeti ya kupewa fedha ya ukamilishaji wa zahanati hiyo ya Gwata. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Nandwahi ambacho kipo Jimbo la Newala, wananchi waliwekeza fedha zao nyingi kwa ajili ya kukiboresha. Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo kile ili kurahisisha huduma za tiba kwa wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala Vijijini, kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo hicho cha afya na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ikihusisha mpango wa mapato ya ndani kuchangia shughuli hiyo ya ujenzi. Vilevile, Serikali kuu itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo hicho cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 6

**Njia Mbadala ya Kukuza Uchumi wa Wananchi wa Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je serikali ina mpango gani wa njia mbadala ya kukuza uchumi wa wananchi wa Hai kutokana na uhaba wa ardhi ya uzalishaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kukua kiuchumi wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Hai. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

Kutoa Mikopo yenye riba nafuu hususan kwa wanawake, vijana na walemavu; Kujenga mfumo wa kidijitali vijijini ili kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kiuchumi; na Kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji, hasa katika Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Hai, Serikali imeendelea kuhakikisha Mradi wa Kiwanda cha *KMTC (Kilimanjaro Machine Tools Company)* ambacho kiko chini ya *NDC* unatekelezwa. Aidha, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hai imetenga eneo maalum la uwekezaji lenye ukubwa wa hekta 463 ambalo linaendelea kutangazwa kwa wawekezaji mbalimbali. Hivyo, Serikali itaendelea kuhimiza na kutangaza fursa

zinazopatikana katika Wilaya ya Hai ikiwemo fursa za Utalii ili kuimarisha uchumi wa wananchi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, sehemu kubwa ya ardhi ya Wilaya ya Hai, iko kwenye mashamba 17 yaliyoko kwenye vyama vya ushirika. Je, Serikali haioni iko haja ya kufanya tathmini ya ardhi ya mashamba haya yote 17 ili tunapoingia mikataba, tuingie mikataba tukihusianisha na thamani ya ardhi tulionayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; moja ya sababu inayosababisha kufifisha uchumi wa Jimbo la Hai ni wawekezaji wasio na uwezo wanaoingia mikataba kwenye mashamba haya ya ushirika. Kwa mfano, shamba la Makoa, Kijiji cha Uduru ni miaka minne shamba lile limesimama, mwekezaji halipi chochote, mwekezaji ni migogoro kila siku ni Mahakamani na wanachi wanakosa uchumi kwenye shamba hilo. Shamba la Mrososangu mwekezaji ameingia mkataba ajenge kiwanda cha parachichi mpaka sasa hivi hajafanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali, najua kuna presha ya uchaguzi, twende kwenye swali. *(Kicheko)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni haja ya kuingilia migogoro hii iliyopo kwenye mashamba ya ushirika ili uchumi wa Jimbo la Hai ambao unategemea kwa kiwango kikubwa sana haya mashamba 17? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Saashisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru na nimpongeze kwa kweli amekuwa ni championi mkubwa anayefuatilia masuala ya ushirika katika wilaya yake na kwa kweli

ni Mbunge ambaye yuko makini nashukuru sana kwa hilo nampongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba 17 yaliyoko chini ya ushirika ikiwa ni pamoja na hayo mashamba ambayo yako chini ya mkataba wa huyu mwekezaji, Ofisi ya Rais masuala ya uwekezaji, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, katika bajeti inayofuata ya mwaka huu tumeweka mkakati mkubwa ambao tutakwenda kufanya tathmini ya mali zote ambazo ziko chini ya *TR* na mali zote ambazo ni za Serikali, kuzifanyia tathmini ya kina kujua thamani ili tunapoingia mikataba ya uwekezaji tuweze kujua tunaingia mikataba katika ardhi au mali ya Serikali yenye thamani ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mkakati upo, Bunge likitupitishia bajeti tutakwenda kufanya kazi hiyo ya tathmini na hii itakuwa ni hatua moja nzuri sana ya kuweza ku-*move* mbele kuweza kuangalia namna ya kuingia mikataba ambayo ni yenye tija, mikataba ambayo inakuwa na manufaa na Serikali. Kwa hiyo, nimtulize Mheshimiwa Mbunge atulie tunakwenda kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa hizi kesi ambazo ziko mahakamani ninasita kuongea kwa sababu ziko mahakamani, basi ni vizuri kuchukua hatua stahiki ili tuweze kuona ni namna gani ya kuweza kwenda mbele katika kuleta tija pande zote mbili kati ya mwekezaji pamoja na wananchi wa Hai. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kutangaza fursa nyingi za uwekezaji zilizoko Mkoani Manyara, ikiwa ni pamoja na kilimo cha ngano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa majibu yangu ni ule ule kwamba tunakwenda kufanya tathmini kubwa ya mali zote za Serikali yakiwemo mashamba, vilevile kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mkoa pamoja na Sekretarieti za Wilaya kuangalia namna ya kuweza kuonesha fursa za uwekezaji katika maeneo hayo. Tutakwenda kutafuta wawekezaji wa ndani na nje kuwawekea mazingira mazuri ya kuwekeza katika fursa tofauti tofauti katika mikoa yetu ambayo iko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa kila mkoa una fursa zake za kiuwekezaji, ni namna bora tu ya kukaa na kuangalia ni fursa zipi tuwape wawekezaji ili waweze kuwekeza na wananchi wa maeneo hayo waweze kupata tija katika uwekezaji huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kyerwa kutokana na uoto wa asili na ardhi yake ina fursa nyingi za kibiashara, lakini inabaki kuwa maskini. Ninataka nijue mkakati wa Serikali kwa kutumia Mto Kagera ili wananchi waweze kuwekeza kwenye vizimba, iweze kusaidia kuongeza uchumi, kipato cha wananchi, uwezo, nia na nguvu wanaweza kufanya hivyo? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu tumekuwa sasa katika utaratibu wa kuandaa dira ya mwaka 2050 baada ya kumaliza dira ya mwaka 2025 ambayo inakwisha mwakani yaani bajeti hii tunayokaa ni bajeti ya mwisho. Naomba nikuhakikishie tumeweza

ku-*identify* na kuangalia kwa kupitia ushauri wa wananchi, tumeweza kuangalia namna ya kwenda kuziwezesha zile sekta ambazo ni za kimkakati ambazo zitakwenda kusaidia kutengeneza na kuongeza uchumi wa nchi yetu, wakati huo huo kutengeneza fursa za ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maeneo ni ya kilimo, uchumi wa bluu na haya yote yanakwenda kufanyiwa kazi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunayo mikakati mizuri ya kuhakikisha kila sekta ambayo tunaona ina tija katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu, ikiwemo masuala ya kilimo na mambo mengi, tunakwenda kuyafanyia kazi vizuri na fursa zitakwenda kufunguka za kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mkenge kwa niaba yake Mheshimiwa Twaha.

Na. 7

**Hitaji la Umeme Kitame – Bagamoyo**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE K.n.y. MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini umeme utapelekwa katika eneo la Kitame, Kata ya Makurunge ili kuwasaidia wazalishaji wa chumvi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Bagamoyo, Serikali kupitia *REA* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya migodi midogo yakiwemo maeneo ya wazalishaji wa chumvi kupitia mkandarasi aitwaye *Dieynem Company Limited*. Hadi kufikia mwezi Machi 2025, jumla ya maeneo 14 ya migodi midogo imepelekewa umeme ambapo kati ya hayo, maeneo matatu ni ya wachimbaji wa chumvi wanaopatikana katika eneo la Kitame Kata ya Makurunge, ambapo jumla ya wachimbaji 34 wanaopatikana katika maeneo hayo wamefikiwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme kwa wachimbaji wa chumvi waliosalia itaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na jitihada kubwa zilizofanyika kuweza kupeleka umeme kwa wachimbaji wa migodi wale wadogo wadogo lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kupeleka umeme kwenye Kitongoji cha Kitame ili wananchi waweze kunufaika katika nyumba zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; zaidi ya shilingi bilioni 3.8 zimetumika pale katika Jimbo la Kibiti kupeleka umeme katika zile Kata Delta, Kata ya Kiongoroni, Mbuchi, Maparoni na Msala. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibiti naomba Mheshimiwa Waziri tufikishie salamu zetu na pongezi kwa Mheshimiwa Rais ili alivyoweza kufanikisha ndoto za wanakibiti wanaoishi katika maeneo ya Delta kuweza kupata umeme.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika eneo hili la Kitame tunayo miradi ya vitongoji ambayo inafuata, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wa Kitongoji hiki na wenyewe watanufaika na huduma hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea salamu za Mheshimiwa Mbunge kwa kweli ni pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa inayofanyika katika Sekta ya Nishati ambayo inasimamiwa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Mashaka Biteko. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama kituo cha kupoozea umeme kilichoko eneo la Uhuru Wilaya ya

Urambo kimekamilika, je, ni lini kituo hicho kitazinduliwa rasmi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tarehe 26 Machi, tuliwasha kituo cha kupooza umeme cha Uhuru *Substation* na kwa sasa hivi wananchi wananufaika kupitia *feeder* ambazo tumezipeleka katika maeneo ya Kaliua pamoja na Urambo.

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu amesikia ombi la Mheshimiwa Mbunge na kwa hiyo nina uhakika tutaweza kulichakata na kulifanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lini mchakato wa umeme katika vitongoji 15 utaanza, ukizingatia katika Jimbo la Kilombero kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa umeme katika Kata ya Michenga, Vitongoji vya Tupendane na Upendo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi wa kupeleka umeme katika vitongoji 15 katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge ameshapatikana na ameshaanza kazi katika maeneo mengine. Tunaendelea kumsisitiza mkandarasi aongeze magenge na aongeze nguvu ili kuweza kufikia Majimbo mengine katika Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kumsimamia mkandarasi huyo ambaye ameanza katika maeneo mengine kwa kadri ya maelekezo ya *RCC* ambayo walikuwa wamekubaliana na baada ya hapo atafika kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Na. 8

**Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji ya Udimaa na Mbwasa – Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji ya Udima na Mbwasa – Manyoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kutekeleza miradi mbalimbali ya umwagiliaji nchini zikiwemo Skimu za umwagiliaji za Udimaa na Mbwasa zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa Skimu za Udimaa na Mbwasa kwa ajili ya ujenzi. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa Skimu ya Mbwasa umekamilika mwezi Februari, 2025 na mkandarasi amekabidhiwa eneo la mradi. Aidha, Skimu ya Udimaa ilitangazwa kwa ajili ya kupata mkandarasi ila taratibu za manunuzi hazikukamilika. Skimu hiyo imetangazwa tena ili kumpata mkandarasi ambaye atakamilisha ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa miradi hii kutanufaisha wakazi zaidi ya 13,000 wa Vijiji vya Kintinku, Mbwasa, Mwiboo, Chikuyu, Chilejeho na Mtiwe vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Daktari Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika Kata ya Sanza iliyoko Halmashauri ya

Wilaya ya Manyoni kuna mto mkubwa ambao unamwaga maji kwenye vijiji vinne na ni *potential* kwa kilimo cha umwagiliaji. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaanzisha Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Sanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika Kata ya Makulu iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, kuna Skimu ya Umwagiliaji ya Msemembo ambayo imeharibika ndani ya miaka mitatu. Sasa nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawanusuru wakulima hao? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Pius Chaya kwa kufanya kazi nzuri kwa wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki. Jambo moja ambalo nimthibitishie ni kwamba, katika huu mkakati wa kuanzisha Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Sanza tuko katika hatua ya upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya baada ya hapo tutatangaza mkandarasi ili aweze kupatikana na kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho kwenye mradi ya Msemembo hayo yapo katika mpango wetu na katika kila mwaka wa fedha tunatenga fedha kwa ajili ya ukarabati. Kwa hiyo na jambo hilo vilevile tutalitekeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Isebya na Kata ya Bugerenga Wilayani Bukombe miradi hii miwili haijapatiwa fedha. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili miradi hii iweze kutengenezwa na wananchi waweze kupata manufaa?

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Isebya inayo Mradi wa Skimu na Kata ya Bungerenga, lakini miradi haifanyi kazi. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili miradi hii ianze kufanya kazi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Miradi miwili aliyoitaja ikiwemo ya Isebya na Bungerenga ambayo bado hatujapeleka fedha, tayari Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tumeomba fedha Wizara ya Fedha ambayo wameahidi kutukamilishia kati ya mwezi huu Aprili na mwezi Mei. Kwa hiyo, fedha hizo zitakapofika maana yake tutapeleka ili ile miradi iendelee kutekelezwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kikwete, jiandae Mheshimiwa Butondo. Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana katika ustawi wa chakula katika Taifa letu la Tanzania. Je, kutokana na skimu za umwagiliaji ambazo zinaleta tija, sisi tunalo Bonde la Kinyope, ni lini fedha zitapelekwa ili tuweze kuanza hiyo kazi, kwa sababu bonde hili lina watu wengi zaidi ya 25,000? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mama Salma Kikwete Mbunge wa Jimbo la Mchinga kwamba, moja ya kazi kubwa ambayo Wizara ya Kilimo tunaifanya sasa ni kufanya usanifu wa kina katika mabonde yote ikiwemo Bonde la Kinyope, baada ya kukamilika kwa bonde hili maana yake tutatafuta fedha ili ziweze kupelekwa pale na ujenzi uanze kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Jimbo la Mchinga. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia eneo la umwagiliaji wamefanya upembuzi wa kina kuhusiana na ujenzi wa Bwawa kubwa la Lunguya katika Kata ya Talaga na tulitarajia kwamba zoezi la ujenzi lingeanza kabla ya mwaka wa fedha haujakwisha. Je,

Serikali inasema nini kuhusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa ajili ya kilimo cha mpunga? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, katika Bonde la Lunguya lililopo katika Jimbo la Kishapu ni kweli Wizara tunalifahamu na tunafanyia kazi. Jukumu kubwa ambalo tulilonalo sasa hivi ni zile fedha ambazo tumeomba Wizara ya Fedha, tukishapata zile fedha maana yake tutapeleka katika maeneo yote ambayo yamepangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, bonde lako pia liko katika mpango huo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea muda wetu unakwenda, Wizara ya Maji Mheshimiwa Hassan Kungu. Mheshimiwa Thea Ntara kwa niaba ya Mheshimiwa Hassan Kungu.

Na. 9

**Hitaji la Maji Kata ya Matemanga**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mradi wa Maji Kata ya Matemanga katika Vijiji vya Milonde, Matemanga na Changarawe – Tunduru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Milonde, Matemanga na Changarawe vilivyopo Kata ya Matemanga Wilayani Tunduru vinapata huduma ya majisafi na salama kupitia vyanzo vya maji vya Mkwinda na Namalowe. Mradi huo ulijengwa mwaka 1980 na baadaye kwa nyakati tofauti kufanyiwa ukarabati katika vipindi viwili tofauti vya mwaka 2012 na 2021 ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma wa skimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya ongezeko la mahitaji ya huduma ya maji kwa wananchi wa Kata ya Matemanga kutokana na ongezeko la idadi ya watu ambapo kwa sasa imefikia zaidi ya watu 10,000. Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026, itajenga tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 500,000 ili kuongeza uzalishaji kutoka lita 275,000 za sasa kwa siku na kufikia lita 775,000. Lengo ni kuhakikisha wananchi wa Kata ya Matemanga wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo majibu aliyatoa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini ahadi ya maji aliyoitoa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa mwaka 2017 itatekelezwa katika Kata Kalulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wa Kata ya Maposeni ikiwemo Kijiji cha Mdunduwaro wana hamu sana ya kupata maji. Je, ni lini sasa mradi huo utakamilika? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Ntara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa upande wa Tunduru Kaskazini Serikali inaendeleza miradi saba, miradi yenye gharama ya bilioni 2.146, katika miradi hiyo miradi miwili imeshakamilika. Tunatambua kwamba, ahadi za viongozi wa kitaifa inaendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha na mradi huu kwa Wizara ya Maji ni kipaumbele, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba huu mradi ni kipaumbele katika Sekta yetu ya Maji kuhakikisha kwamba unakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika eneo la Mdunduwaro ambalo liko katika eneo la Songea tayari tulishapata Mkandarasi na tunaamini kwamba bado yuko ndani ya mkataba wa utekelezaji wake, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo, mradi huu utakamilika na utatoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kupeleka mradi wa maji Kijiji cha Hunyari kwa shilingi milioni 830, lakini mpaka leo wananchi wa Hunyari wanapata shida juu suala la maji. Je, ni lini Serikali itakamilisha huu mradi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Getere kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wake. Pili, nampongeza kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ikiwemo kupeleka fedha ambazo ni shilingi milioni 830 katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo alilolitaja, changamoto iliyopo pale ni pampu ambayo ilikuwa inatumika kusukuma maji, bado inadaiwa kiasi cha shilingi milioni mia mbili na thelathini na kitu, ambapo Wizara ya Maji imeishapokea na inalifanyia kazi. Litakapokamilika, huduma ya maji itaanza kutoka katika eneo hilo bila kuwa na shaka yoyote, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Mradi wa Kata ya Boma la Ng'ombe utakamilika kwa sababu, wananchi wa kata hiyo wamekuwa wakiusubiri kwa muda mrefu, ili kumtua mwanamke ndoo kichwani na kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge kutoka Mkoa wa Iringa. Eneo la Boma la Ng'ombe, tayari Serikali imeishapeleka fedha na mradi huu umeshaanza kujengwa na tumeshakamilisha tenki na sasa kazi iliyobaki ni kuunganisha huduma ya nishati ya umeme ili sasa zile pampu ziweze kuanza kusuma maji. Wananchi ambao Mheshimiwa Ritta Kabati anaendelea kuwapigania, basi watapata huduma ya maji safi na salama, ili waweze kuendelea kushuhudia makubwa yanayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Nusrat

Na. 10

**Uhitaji wa Maji Safi na Salama Sambaru, Mang'onyi**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, lini Wananchi wa Kijiji cha Sambaru, Kata ya Mang'onyi, Singida Mashariki, watapata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Sambaru kilichopo Kata ya Mang'onyi, Wilayani Ikungi, kinapata huduma ya maji safi na salama kupitia Skimu ya Maji ya Sambaru iliyojengwa mwaka 2003, kwa ajili ya kuhudumia watu 4,048 wa kijiji hicho. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, kijiji hicho kinakadiriwa kuwa na watu 6,830, hivyo kuwa na ongezeko la mahitaji ya maji ukilinganisha na huduma inayotolewa kupitia miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Serikali imekamilisha uchimbaji wa kisima kirefu chenye uwezo wa

kuzalisha maji lita 2,800 kwa saa. Aidha, kwa sasa zoezi la ujenzi wa *point source* ya kutolea huduma kwa wananchi linaendelea. Sambamba na hilo, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itatenga bajeti zaidi kwa ajili ya utafutaji wa vyanzo vya maji vya uhakika katika kijiji hicho kwa lengo la kuboresha huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mechi ya Simba ni kesho.

**MBUNGE FULANI:** Ehee! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sioni sababu ya watu wasiohusika na Simba ndiyo wanazungumza zaidi humu ndani. Mheshimiwa Nusrat. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na kwamba, Serikali inaendelea na zoezi la kuchimba visima, hususan katika Kijiji hiki cha Sambaru kwenye Kata ya Mang'onyi, bado kuna changamoto ya miundombinu ya usambazaji wa maji, kikiwemo kisima hiki kilichochimbwa juzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna kata nyingine ambazo visima vimechimbwa, lakini bado hakuna miundombinu ya usambazaji wa maji, kikiwemo Kijiji cha Msule, Kijiji cha Sakaa pamoja na Kijiji chenyewe cha Misughaa, kwenye Kata ya Misughaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kwa nini Serikali wakati inaweka mipango ya kuchimba visima isiunganishe na *package* ya usambazaji wa maji ili isiwe tu tunasema kwamba tumechimba visima kadhaa na tutaendelea kutafuta vyanzo, tuwe tunaweka kabisa, ili tuhakikishe maji yanawafikia wananchi kama ambavyo tumewaahidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna mradi ambao unaendelea kuzinduliwa katika mikoa kadhaa nchini, mradi wa visima 900. Nilikuwa nauliza, katika jimbo letu la Singida Mashariki, ikiwemo Wilaya ya Ikungi, majimbo yote mawili, Mkoa wa Singida

kwa ujumla, nataka nifahamu kama mkoa wetu pia umo katika huu mradi wa visima 900? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali zuri kabisa kutoka kwa Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kazi kubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaifanya, akiwemo Mheshimiwa Nusrat, ya kupambania akina mama wanaohitaji kutuliwa ndoo kichwani. Ni programu ambayo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais, lakini visima 900 ni visima ambavyo vinachimbwa nchi nzima katika mikoa yote ya Tanzania Bara na vilevile kwa upande wa Singida imo katika programu ya visima hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na Mkoa wa Singida ulitengewa shilingi bilioni 18.6, kwa ajili ya miradi 43 inayotekelezwa katika Mkoa wa Singida. Vilevile visima hivi, zaidi ya 636, tayari vimeishapata maji na vingine tunaendelea kujenga zile *point source* ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge ameulizia, kwamba tunapochimba visima tuwe na *package* moja kwa moja ya usambazaji; tunachokifanya kwanza kabisa ni kuchimba ili kuona kama kuna maji. Pili, tunafanya *test* ya pampu kujua wingi wa maji, ili tuweze kujua ni pampu ya aina gani au miundombinu ipi tutakayoiweka pale, ifikie idadi ipi ya watu kulingana na maji ambayo tumeyapata?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba wananchi wote ambao wamezunguka maeneo hayo tunawafikishia maji kulingana na idadi, kulingana na kiu ya maji ambayo tumeipata na kulingana na kisima ambacho tumekichimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Serikali imejipanga kwenye kuchimba, kujenga

miundombinu, usambazaji wake na utoaji wa huduma yenyewe ya maji; yawe safi na salama na yenye kutosheleza, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Ni kwamba, Wizara ya Maji ilileta roli kwa ajili ya kuchimba visima 39 katika Wilaya ya Sengerema, hasa Jimbo la Sengerema na gari lilikuwepo pale kwa ajili ya kuchimba visima hivyo, lakini lile gari lilitoroshwa usiku. Ni lini hilo gari litarudishwa Sengerema, kwa ajili ya kuja kufanya kazi ya kuchimba visima? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika kuhusu utoroshwaji wa gari, lakini natambua uhitaji wa gari hilo ili wananchi wa Sengerema wachimbiwe visima na wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kukamilisha tenki la ujazo wa lita milioni tisa kule Bangulo na sasa wanaanza usambazaji wa maji katika maeneo mbalimbali. Je, ni ipi *commitment* ya Serikali kwenye kumaliza usambazaji wa maji katika Mtaa wa King'azi A na B, Mtaa wa Saranga na Mtaa wa Ukombozi ili wananchi hawa sasa wafurahie maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mtemvu kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wa Kibamba. Ni kweli kabisa utekelezaji wa ujenzi wa tenki hili la lita milioni tisa, Mheshimiwa Mbunge tumekuwanaye wakati tunakagua mradi huu na sasa umeshakamilika katika ujenzi wake, lakini sasa zoezi linalofuatia ni

kusambaza maji katika maeneo yote, ambapo katika *study* iliyofanyika ni kwamba maeneo yote ambayo yanaguswa yatafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda hatua kwa hatua kulingana na hali halisi ya upatikanaji wa fedha. Lengo ni kwamba, tunapofika Oktoba, 2025 basi wananchi wawe wamepata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutekeleza miradi ya maji katika Mkoa wetu wa Mara, lakini ningependa kujua sasa ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa maji kutoka Musoma Mjini kuelekea Wilaya ya Butiama katika Kata ya Bisumwa – Nyankanga na Bukabwa ili wananchi wale waweze kupata maji hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ghati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma ya maji safi na salama. Maji yapatikane, maji yafikike na maji yaweze kunyweka yakiwa na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Musoma, tayari Serikali imeshatekeleza miradi kadhaa chini ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini mradi mmojawapo wa Mugango – Kiabakari ambao ulikuwa ni kizungumkuti, umeshakamilika na umeshaanza kutoa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, tunaamini kwamba katika maeneo ambayo yamebaki, yakiwemo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kufikisha huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Saada Monsour Hussein. *(Makofi)*

Na. 11

**Changamoto ya Vituo vya Polisi na Vitendea Kazi Kaskazini Unguja**

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya Vituo vya Polisi na vitendea kazi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kaskazini Unguja una wilaya mbili; za Kaskazini A na Kaskazini B, zenye jumla ya Vituo vya Polisi viwili Daraja A, Daraja B vituo vitatu, Daraja C kituo kimoja na kuna vituo viwili vya Polisi vya Tumbatu na Pwani Mchangani ambavyo vinaendelea na ujenzi. Mkoa huu una jumla ya magari ya Polisi 15 na pikipiki 22 zinazofanya kazi mbalimbali za Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kaskazini A kuna magari matatu na pikipiki nane, na katika Wilaya ya Kaskazini B kuna magari mawili na pikipiki tisa. Serikali kupitia Halmashauri za Mji na Wilaya, zitaendelea kutoa maeneo kwa ajili ya kujenga Vituo vya Polisi, ikiwa ni pamoja na Serikali kutenga fedha toka kwenye Bajeti ya Serikali kila mwaka, kwa ajili ya kujenga Vituo vya Polisi na kununulia vitendea kazi kama magari na pikipiki, ili kutoa huduma bora kwa wananchi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saada.

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa maswali mawili ya nyongeza, na pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Swali langu la kwanza ni kwamba, Kituo cha Polisi Kiwengwa kina

hali mbaya. Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati kituo hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa, wananchi wa Vijiji vya Kichwele, Kichungwani, Muembe Majogoo, Mchanjarike na Kitopendani, wanatembea umbali mrefu kufuata Kituo cha Polisi Mahonda. Je, ni lini Serikali itawajengea Kituo cha Polisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mbunge wa Viti Maalum kwa ufatiliaji wake makini. Kwa swali la kwanza kwamba Kituo cha Polisi alichokitaja hali yake ni mbaya; nimhakikishie kwamba, Serikali inafanya tathmini ya kuona uchakavu wa vituo vya Polisi na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu mahitaji ya Kituo cha Polisi kwenye eneo ambalo amelitaja, Serikali imetenga Ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Kata na Shehia awamu kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba kituo alichokitaja pia, kitawekwa kwenye mpango, tayari kwa ajili ya utekelezaji, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq, jiandae Mheshimiwa Kandege.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Kituo cha Polisi katika eneo la Kizota, ambacho kimeanza kujengwa miaka miliwi na nusu iliyopita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kazi iliyofanywa, na kituo kimefikia hatua nzuri. Niagize Jeshi la Polisi, kupitia, kufanya tathmini ya kiwango

kilichofikiwa na kutenga fedha kwa ajili ya umaliziaji wa hiki Kituo cha Polisi cha Kizota, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege, jiandae Mheshimiwa Kunti.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Katika wilaya chache ambazo hazina Vituo vya Polisi ni pamoja na Wilaya ya Kalambo. Je, ni lini Serikali watajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Kalambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kalambo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wilaya ya Chemba tumejengewa Kituo bora cha Polisi cha Wilaya, lakini hatujakamilisha ununuzi wa samani za ofisi. Ni lini Serikali itakamilisha ununuzi wa samani za ofisi ili ofisi ile ianze kutumika kwa ajili ya kuhudumia wananchi kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niwapongeze kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chemba, ambacho kimekamilika. Nimhakikishie Mheshimiwa Kunti kwamba, katika mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026, tutatenga fedha kwa ajili ya kununua samani ili kituo hicho kifanye kazi kama ambavyo imekusudiwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Zacharia kwa niaba ya Mheshimiwa Regina.

Na. 12

**Kupunguza Gharama za Kusafisha Figo Nchini**

**MHE. REGINA N. QWARAY K.n.y. MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama ya matibabu ya kusafisha figo katika hospitali zetu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kupunguza gharama za kusafisha figo, ikiwa ni pamoja na kusogeza huduma hizi kwa kuongeza vituo vya *dialysis* katika hospitali 15 za rufaa za mikoa, na hospitali zote za kanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali itaongeza wadau na taasisi zinazoingiza vitendanishi, vifaatiba na dawa zitumikazo badala ya kuacha mtu mmoja au taasisi kutawala soko bila kuruhusu ushindani na pia kuhamasisha viwanda na ubunifu ndani ya nchi. Aidha, Serikali imesambaza kwenye hospitali za rufaa za mikoa nchini mashine zaidi ya 100 pamoja na vitendanishi vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa wananchi, mara utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote utakapoanza, waweze kujiunga, kwani ndiyo njia pekee ya kuweza kuwasaidia kuepukana na gharama za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru sana Serikali kwa kutuletea huduma hii katika ngazi ya Mkoa na tayari Mkoa wa Manyara tumepokea vifaa, lakini

pamoja na vifaa hivyo kufika ngazi ya mkoa kulingana na jiografia ya mkoa wetu, bado baadhi ya Wilaya zitakuwa katika umbali mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kusogeza huduma hizi katika ngazi za wilaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa ya figo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaandaa watalamu wa kutosha ili kuweza kutoa elimu kwa wananchi waweze kuepukana na ugonjwa wa ufigo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge Regina Ndege kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia masuala ya afya kwenye maeneo ya Mkoa wa Manyara. Amekuwa akifuatilia kwenye wilaya mbalimbali akishirikiana na Wabunge wa Majimbo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, maswali yake mawili ya msingi ni kwamba sasa tumefika kwenye hospitali 15 za mikoa, tutaenda kumalizia hospitali zote kwa sababu kuna utaratibu wa kusomesha watalamu kupitia Mfuko wa Rais Samia *Scholarship,* na wataalamu watakapopatikana, basi tutawashusha. Watakapokuwepo wataalamu wenye uwezo ndani ya halmashauri zetu na kila Wilaya, sasa tutaanza kwenda pole pole na wilaya ziwezeshwe kufanya huduma kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili juu ya suala la kutoa elimu, mimi nipokee, na kwa kweli kuna wataalamu. Sisi tutakachoongeza ni kwamba, hata kwenye kliniki, kila mahali ambapo elimu inatolewa kuhusu magonjwa mengine, tutahakikisha hatusahau kutoa elimu kuhusu matatizo ya figo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe, hayupo!

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Habari na Utamaduni, Mheshimiwa Toufiq kwa niaba Mheshimiwa Amina.

Na. 13

**Ongezeko la Vyombo vya Habari Mtandaoni**

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha ongezeko la vyombo vya habari mtandaoni haliathiri maadili na utamaduni wa Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* imeendelea kutoa leseni za vyombo vya habari na waandaaji wa maudhui mtandaoni kwa maombi ambayo yanakidhi vigezo vilivyowekwa ili kupanua wigo wa kutoa habari nchini kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utangazaji. Hadi Machi, 2025, leseni 206 za televisheni na redio za mtandaoni zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TCRA* imeendelea kutoa elimu na imekuwa na programu maalumu za kuwaelimisha watumiaji wa mitandao kuhusu matumizi sahihi na salama ya mitandao. Pia, kuendelea kufuatiilia wale wanaokiuka maadili ya Mtanzania na kuwawajibisha, ikiwemo kufungia uzalishaji wa maudhui na kuwapiga faini kwa mujibu wa Sheria za Vyombo vya Habari na za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hayo, Serikali imeanzisha Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, bodi hii inasimamia weledi na maadili kwa waandishi, na kuhakikisha waandishi wenye sifa tu ndio wanaoruhusiwa kutumika katika vyombo vya habari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Kumekuwa na ongezeko kubwa la vyombo vya habari vya mtandaoni. Je, Bodi ya Ithibati inasimamiaje kuhakiki waandishi wa habari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Ithibati lengo lake la msingi litakuwa ni kuhakikisha kwamba inasimamia weledi na maadili miongoni mwa waandishi wa habari, wakiwemo waandishi wa habari wa vyombo vinavyotekeleza majukumu yake mtandaoni. Itakuwa na jukumu la kusimamia vyote hivi ili kuhakikisha kwamba waandishi wa habari wanafanya shughuli zao kwa kufuata weledi, maadili, na kuzingatia usalama wa Taifa bila kukandamiza uhuru wa habari.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

Na. 14

**Hitaji la Kiwanda cha Asali Sikonge**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaona haja ya kuwa na kiwanda cha asali Tarafa ya Kiwele – Sikonge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Sikonge ina tarafa mbili ambazo ni Tarafa za Sikonge na Tarafa ya Kiwele. Serikali kupitia Mfuko wa Huduma za Misitu Tanzania *(Tanzania Forest Services)* ilijenga kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki Tarafa ya

Sikonge. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuchakata asali tani nne kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukidhi mahitaji ya kiwanda kilichojengwa, sasa Serikali itaanza mchakato wa awali wa kujenga kiwanda cha pili cha kuchakata mazao ya nyuki, ikiwa ni pamoja na kuainisha uwezo wa uzalishaji wa asali kwa Tarafa ya Kiwele, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Kama alivyosema, kuna kiwanda ambacho kimejengwa Wilaya ya Sikonge, lakini tangu kizinduliwe kiwanda kile hakijaanza kufanya kazi. Je, ni lini Serikali itaweza kuamua kiwanda hicho kiweze kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kutoka Tarafa ya Kiwele kwenda Makao Makuu ya Wilaya ni takribani kilometa 300, na tarafa ile ina uzalishaji mkubwa sana wa asali. Je, Serikali haioni kuna haja kubwa ya kuweka kiwanda maeneo yale pia, kwani labda ndiyo sababu inayopelekea kiwanda cha Sikonge kishindwe kufanya kazi kwa haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jacqueline kwa kazi nzuri anayoifanya ya kufuatilia sekta hii ya asali katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafuatilia, lakini taarifa za awali zilizonesha kuwa kulikuwa na changamoto za uendeshaji wa kiwanda kile cha awali cha Sikonge ambacho tulizindua mwaka 2023 chini ya Mheshimiwa Kakunda ambaye alifanya kazi kubwa sana kuvutia pale Sikonge kujengwa kiwanda hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutafuatilia tuone changamoto ni nini? Pamoja na hayo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kweli tutajiridhisha kuwa kulingana na

umbali huo aliousema kutoka Kiwele mpaka Kiwanda hiki cha Sikonge, na kama uzalishaji ni mkubwa na wa kutosha kuweza kuvutia wawekezaji katika Tarafa hii ya Kiwele, namhakikishia Mheshimiwa Jacqueline kwamba tutafanya hivyo kwa sababu tayari kuna wawekezaji wengi ambao wako tayari kujenga viwanda kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutafanya hivyo ili kurahisisha uchakataji wa asali katika tarafa hii ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia, ahsante.

**NAIBU SPUIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu na Sayansi, Mheshimiwa Dkt. Nahato.

Na. 15

**Uhaba wa Mabweni Vyuo Vikuu vya Umma**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza uhaba wa mabweni katika vyuo vikuu vya umma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa malazi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya umma nchini. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa mabweni mapya 26 katika kampasi 12 za vyuo vikuu vya umma nchini. Mabweni haya yakikamilika yatakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 5,987 kwa wakati mmoja. Ujenzi wa majengo ya mabweni hayo unatarajiwa kukamilika mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inatoa wito kwa sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa *hostel* katika maeneo ya vyuo vikuu ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya malazi kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Nahato.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, hasa pale aliposema kwamba sekta binafsi iwekeze. Hapo nimepapenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza. Mwezi wa Tano, wanafunzi wa *Form Six* wanamaliza mitihani, na mojawapo ya ufaulu wa wanafunzi ni uhakikisho wa sehemu wanakolala. Je, tumejipanga vipi hao wanafunzi wakimaliza mitihani waweze kupata sehemu za kulala, wajue kabisa wanakwenda chuo fulani na wanapata mahali pa kulala? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mloganzila ni eneo kubwa sana na ina hospitali. Kwa nini tunabanana pale Muhimbili? Eneo kubwa lile la Mloganzila lingetumika. Basi hao wawekezaji wapewe hilo eneo wajenge mabweni mengi sana ili wanafunzi wetu wapate mahali pa kukaa, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Nahato, kwamba naye ni mpiganiaji sana ya maslahi ya vyuo vikuu hapa nchini. Kwamba, tunahitaji kuwa na uhakika zaidi wa sehemu za kulala, kwa sasa hivi chuo ambacho tuna uhakika 100% wanafunzi wakienda wanaweza wakapata sehemu za kulala ni *UDOM,* Chuo Kikuu cha Dodoma. Vyuo vingine ni wastani wa 30% mpaka 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la swali la awali, ni kwamba, Serikali sasa hivi inawekeza sehemu mbalimbali kwa ajili ya kuongeza na kupanua wigo wa kampasi za kulala, na vilevile kuvutia hata kwenye utaratibu wa *PPP*, sekta binafsi kuja kuwekeza kwa ajili ya kuwa na *hostel* za wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la nyongeza, Mloganzila ni pakubwa, ni kweli, na tayari napo ni

sehemu ambapo tunajenga, tunafanya upanuzi kwa ajili ya kuongeza makazi ya wanafunzi. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya dharura, hoja ya dharura!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, sasa ni kipindi cha kutangaza wageni.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; mgeni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia, Mheshimiwa Raymond Mwangwala, Mkuu wa Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ndugu Simba Jerry Simba, ni mtoto wake. *(Makofi)*

Kumbe haya majina mnayapenda eeh! Haya. *(Kicheko)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia, kutoka Rombo Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, ambye ni Mchungaji Gregory Malonga kutoka *TAG* Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 34 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 21 na walimu wanne wa Shule ya Awali na Msingi Mirabelle kutoka Kata ya Mkonze Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 72 na walimu nane kutoka Shule ya Msingi Kanosa ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Uongozi kuwa leo Jumanne tarehe 8

Aprili, 2025 kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi kitakachofanyika katika Ukumbi wa Spika uliopo ghorofa ya kwanza, mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa 5.00 asubuhi hii.

Aidha, anaomba awatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, leo tarehe 8 Aprili, 2025 saa 10.00 jioni, utafanyika Mkutano wa *Briefing* katika Ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Kuchauka.

## HOJA YA DHARURA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1), inayohusu kuahirisha shughuli za Bunge kwa muda kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikoa ya Lindi na Mtwara leo ni siku ya tatu mfululizo haina mawasiliano ya barabara baada ya mvua zinazoendelea kunyesha na kubomoa barabara hiyo. Kwa kuwa jambo hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara inapofikia kipindi hiki, basi ikupendeze Bunge lako lijadili jambo hili ili tuweze kuishauri Serikali ione namna bora ya kuliendea jambo hili, na hatimaye kupata ufumbuzi ili wananchi wale waendelee kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kaeni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa, mwongozo wangu unaelekeza Waziri wa Miundombinu wa Wizara ya Ujenzi, Waziri wa TAMISEMI; basi Mheshimiwa Lukuvi jibu kwa niaba ya Serikali.

Taarifa tunazopewa ni kwamba, Serikali iko kazini. Waziri wa Miundombinu, Wizara ya Ujenzi pamoja na TAMISEMI, wote wako *site*. Hiyo ndiyo Serikali makini, inafanya kazi kabla ya hoja. Mheshimiwa kaa chini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.28 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 9 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*